**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BARAZA LA MITIHANI**

**MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A**

**664** **MITAALA NA UFUNDISHAJI**

**Muda: Saa 3.** **Wednesday, 13$^{th}$ Mei 2009**

---

**Maelekezo.**

1. Karatasi hii ina sehemu **A**, **B** na **C.**
2. Jibu maswali **yote** katika sehemu **A** na maswali **mawili (2)** kutoka sehemu **B** na swali **moja (1)** kutoka sehemu **C**.
3. Sehemu **A** ina alama 36, sehemu **B** ina alama 40 na sehemu **C** ina alama 24.
4. Vifaa vya mawasiliano na vitu vyote visivyoruhusiwa **havitakiwi** ndani ya chumba cha mtihani.
5. Andika **namba yako ya mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

maktaba.tetea.org
TETEA


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

**SEHEMU A (alama 36)**

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

1. Fafanua dhana ya Mwanafunzi kama Kielelezo katika mitaala.
2. Bainisha kazi tatu (3) za Kamati ya Mitaala katika shule.
3. Kwa nini upimaji na tathmini ni kipengele muhimu katika ufundishaji na ujifunzaji?
4. Tofautisha njia ya kuigiza na njia ya uigizaji dhima kama mbinu za kufundishia.
5. Orodhesha sifa nne (4) za zana bora ya kufundishia na kujifunzia.
6. Fafanua umuhimu wa maudhui ya somo katika andalio la somo.
7. Eleza maana ya azimo la kazi la kila wiki na taja umuhimu wake.
8. Taja misingi mitatu (3) ya kijamii inayoathiri uundaji wa mitaala.
9. Kwa nini mwalimu anahitaji kujitathmini baada ya kumaliza kipindi cha somo?

**SEHEMU B (alama 40)**

Jibu maswali **mawili (2)** kutoka sehemu hii.

10. Jadili faida nne (4) za kutumia mbinu ya kazi za vikundi darasani na taja mapungufu mawili (2) ya mbinu hiyo.
11. Fafanua kwa kina jinsi azimio la kazi linavyomsaidia mwalimu kuokoa muda na kupanga rasilimali.
12. Wewe ni mwalimu mwanafunzi uliyemaliza mazoezi ya kufundishia. Eleza changamoto nne (4) kuu ulizokumbana nazo na namna ulizitatua.
13. Kwa kutumia somo la Sayansi au Maarifa ya Jamii, tunga zana za kufundishia na kujifunzia ambazo zinalenga milango ya maarifa ya kuona na kugusa kwa wanafunzi.


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

**SEHEMU C (alama 24)**

Jibu swali **moja (1)** kutoka sehemu hii.

14. Jadili mikakati mitano (5) ya kusimamia nidhamu katika darasa la shule ya msingi lenye changamoto.

15. Fafanua umuhimu wa kufundisha kwa vitendo katika kufanya wanafunzi waelewe dhana ngumu.

16. Eleza umuhimu wa kuunganisha masomo katika ufundishaji wa mtaala wa msingi.


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org